Rasimu ya Kwanza

Mwongozo wa Kanuni za Maadili ya Utawala Bora na Uwajibikaji kwa ajili ya the Foundation for Civil Society na Mashirika Wafadhiliwa

Dar es salaam, 23 Februari 2007

1. Utangulizi (Introduction)

Mwongozo wa Kanuni za Maadili Mema ya Utawala na Uwajibikaji ndani ya Shirika la the Foundation na Mashirika Wafadhiliwa (Grantees) ni matokeo ya maoni yaliyotolewa na washiriki wa Tamasha la Jumuiya za Kiraia liliofanyika Agosti 17 na 18, 2006, Karimjee, jijini Dar es salaam. Katika Tamasha hilo mifano ya miongozo ya hapa Tanzania ya: **MS – Tanzania;** rasimu ya Baraza la NGO nchini; Botswana na Uganda ilifafanuliwa ambapo washiriki walionyesha umuhimu wa the Foundation kuwa na kanuni kama hizo. Mwongozo huu unakusudia kuimarisha utawala bora, uwajibikaji, uwazi na uzingatiwaji wa matokeo endelevu katika utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na the Foundation.

Mwongozo huu unahitaji kumilikiwa, kuheshimiwa na kufuatwa na the Foundation for Civil Society na Asasi za Kiraia zinazofadhiliwa na the Foundation. Mwongozi umelenga kuzifanya pande hizi mbili kuwa vyombo vyenye kuzingatia wajibu wao katika jamii, zenye kuwajibika, zenye uwazi, zenye kuzingatia usawa, ufanisi, na matokeo endelevu ya miradi.

Lengo kuu la Mwongozo wa Kanuni hizi za Maadili ya Utawala Bora na Uwajibikaji ni kuimarisha utawala bora na kuzipa kauli zaidi jamii tunazozihudumia ili kuboresha taswira, kuaminika na kusudi la kuwepo kwetu katika jamii.

Kwa kuheshimu viwango vya kanuni na miongozo iliyowekwa katika kanuni hizi za Maadili ya Utawala Bora na Uwajibikaji, the Foundation for Civil Society na Mashirika Wafadhiliwa:

- Tutakuza utamaduni wa kuwajibika kikamilifu katika shughuli zetu zote zinazolenga jamii tunazozihudumia na kuzingatia matokeo endelevu ya kazi zetu, uadilifu, na viwango vya ubora wa juu wa huduma zetu kwa jamii
- Tutazingatia ufanisi ili kufikia malengo tunayojiwekea na kutumia rasilimali fedha kwa umakini wa kiwango cha juu kabisa
- Tutakuza utamaduni wa kuwasaidia walengwa wetu ili washiriki katika michakato ya kufanya maamuzi, ndani na nje ya miradi yetu
- Tutakuza uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi na kutoaji wa taarifa sahihi na pia kupambana na rushwa na utamaduni wa usiri usio na manufaa
- Tutakuza utamaduni wa kubadilishana taarifa na mbinu za utendaji bora
- Tutaheshimu na kuzingatia utoaji wa fursa sawa, na haki kwa makundi yote katika jamii tunazofanyanazo kazi bila ya ubaguzi wa jinsia, asili ya mtu, dini yake, kabila lake, rangi au aina ya ulemavu.

2. Viwango vya Maadili (Standards of Conduct)

zifuatazo zitakuwa ndiyo kanuni za msingi za utekelezaji na mwenendo zinazotumiwa na the Foundation for Civil Society na Mashirika Wafadhiliwa:

2.1 Utawala Bora (Good Governance)

- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa kila mmoja atakuwa na katiba ilizoandikwa ambayo inaainisha bayana shughuli (mission), dira, na malengo na pia kuonesha muundo wa uongozi wa asasi.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutajitahidi kuhakikisha kuna mgawanyo bayana wa madaraka na kazi, kati ya mamlaka za kikatiba za viongozi wa kuchaguliwa/kuteuliwa na maofisa mradi (waajiriwa au wa kujitolea).
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutahakikisha kwamba taarifa zote za bajeti/fedha zinawekwa wazi kwenye ofisi zetu/mbao za matangazo, au maeneo ya warsha pamoja na kusambazwa kwa mamlaka husika katika ngazi mbalimbali za uongozi.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutafuata sheria za kazi za nchi.

2.2 Kipaumbele kwa Watu na Jamii (People Centred and Community Priority)

- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutaziona juhudi zetu kama njia ya kuwezesha jamii kutatua matatizo yao wao wenyewe. Tutasisitiza haki za watu, hususan wale wanaoishi katika mazingira magumu katika jamii, ili washiriki kikamilifu katika michakato ya maamuzi yanayogusa maisha yao.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutahakikisha uandaaji wa miradi inayozingatia mahitaji na vipaumbele vya jamii na ustawi wa mazingira na taifa kwa ujumla.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutahakikisha miradi yetu inapangwa, kusanifiwa, kutekelezwa, na kutathminiwa kwa kuzingatia usawa na ushiriki wa walengwa.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutazingatia mgawanyo wa rasilimali kwa kuzingatia uwiano wa mahitaji ya walengwa (utekelezaji wa mradi husika) na uendeshaji wa asasi (ustawi wa asasi na utawala).
- Tutaheshimu na kuzingatia haki za binadamu zinazotambulika, za kitaifa na zile za kimataifa.

2.3 Mabadiliko kwa Jamii (Impact to Community)

- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutatengeneza viashiria bayana na vinavyopimika kwa ajili ya ajili ya miradi na programu zetu ili kupima umuhimu na manufaa yake kwa jamii.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutaweka wazi matokeo ya tathmini zozote za shughuli zetu kwa umma na kwa watu wote watakaozihitaji.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutaanzisha taratibu stahiki kwa ajili ya tathmini za wenyewe kwa wenyewe (peer review mechanisms) za programu na miradi yetu.

2.3 Mkakati wa Uendelevu (Sustainability Strategy)

- FCS na Wafadhiliwa tutajitahidi kuhakikisha kwamba programu/miradi yetu yote inapangwa kwa kuzingatia matatizo ya jamii. Miradi itakayochukuliwa na jamii lengwa au mamlaka za serikali za mitaa itasanifiwa ili iwe endelevu.
- FCS na Wafadhiliwa tutafanya kazi kwa pamoja kuhakikisha uendelevu wa miradi husika kwa kijamii.

2.4 Mawasiliano, Usambazaji na Upatikanaji wa Taarifa (Communication Dissemination and Access to Information)

- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutashirikiana na kubadilishana taarifa na uzoefu kwa ajili ya kujifunza, kujenga utamaduni wa uwazi na kukuza uelewa wa pamoja.
- Sera muhimu na miongozo ya the Foundation ikiwemo ile ya ruzuku na ile ya Wafadhiliwa itapatikana kwa urahisi na itazingatiwa na wadau husika.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa watafanya mawasiliano katika lugha iliyo rahisi na inayoeleweka (ikiwa ni pamoja na lugha ya ishara) na kutumia tafsiri zilizoandikwa na/za mdomo ili kuhakikisha taarifa zinawafikia wahusika.
- Asasi Wafadhiliwa zitafanya mikutano ya mara kwa mara ya ndani ili kupashana taarifa juu ya shirika na ikiwezekana kusambaza taarifa za maamuzi makubwa kwa wadau husika.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutahamasisha matumizi ya Teknolojia ya Habari (barua pepe na tovuti) kwa ajili ya kuboresha mawasiliano na upatikanaji wa habari.

2.5 Uadilifu, Haki na Usawa (Ethical Integrity, Fairness and Equity)

- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutakuwa wakweli katika shughuli zetu zote na kuepuka matendo ambayo yatadhoofisha uadilifu wa asasi zetu.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutatafuta na kupokea fedha na misaada kutoka katika vyanzo ambavyo malengo yake yanaenda sanjari na kazi na malengo yetu, ambapo misaada hiyo haidhoofishi uhuru na utambulisho wetu.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutatekeleza na kuendeleza haki na usawa kwa wadau, jamii na umma kwa ujumla.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutasisitiza uwiano wa kijinsia, umri (vijana na wazee) na walemavu na kujitahidi kuhakikisha ushiriki sawa wa makundi hayo katika harakati zetu maendeleo.

2.6 Uwazi na Uwajibikaji (Transparency and Accountability)

- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutakuwa wawazi na wenye kuwajibikaji katika shughuli zetu zote na Serikali, Jamii, Umma, Wahisani na wadau wengine.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutatumia fursa zilizopo kama vile ripoti ya mwaka, mbao za matangazo, kuta za ofisi, magazeti n.k. kuutaarifu umma kuhusu kazi yetu, vyanzo vya fedha na matumizi.
- Kwa mujibu wa sheria ya NGO, kifungu cha 29 (a na b) , The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutatoa kwa mamlaka husika, BODI ya NGOs na Baraza la NGOs, taarifa zetu za ukaguzi wa hesabu, na taarifa za kazi zetu za mwaka.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutatengeneza na kufuata miongozo (guidelines) ya fedha ili kusimamia vyema matumizi ya fedha hizo.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutakuwa wakweli na waaminifu katika masuala yote yanayohusiana na ukusanyaji, matumizi na uandaaji wa taarifa za hesabu.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutahakikisha tunatoa ripoti yoyote ya fedha inapoombwa na mdau au mamlaka husika.

2.7 Taratibu za Manunuzi (Standard Procurement Procedures)

- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutahakikisha kuwa manunuzi yanalingana na 'thamani ya fedha' inayotolewa na tutazingatia viwango vya uwazi wa hali ya juu katika michakato ya manunuzi (procurement).
- Kwa manunuzi yoyote yale yaliyo zaidi ya shilingi 500,000 za Kitanzania, The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutahakikisha tunapata nyaraka (quotations) kutoka kwa walau wagavi watatu tofauti.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutahakikisha kuwa watoa huduma (service providers) na mauzo ya vifaa mbalimbali (sales of major equipment) vinafanyika kupitia zabuni za wazi.

2.8 Mapambano Dhidi ya Rushwa (Anti-Corruption)

- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tunatambua kuwa rushwa ni **"matumizi mabaya ya madaraka kwa maslahi binafsi".**
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa hatutajihusisha na mambo ya rushwa.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutatimiza wajibu wetu kila tunapokabiliana na vitendo vya rushwa.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutapenyeza (mainstream) mikakati dhidi ya rushwa katika sera, kazi na programu zetu.
- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutaendeleza dhana na imani ya utumishi uliotukuka na kujituma katika kazi.

3. Uzingatiaji, Ufuatiliaji na Tathmini ya Kanuni Hizi (Code Commitment, Observance and Evaluation)

- The Foundation na Asasi Wafadhiliwa tutajitahidi kuyazingatia maadili haya ya Utawala Bora na Uwajibikaji kwa lengo la kuhakikisha utendaji uliotukuka wa asasi zetu.
- Kanuni za Maadili zitakuwa ni sehemu ya Mikataba ya Asasi Wafadhiliwa. The Foundation na Asasi Wafadhiliwa watatia saini Kanuni hizi kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa.
- Mwezi November kila mwaka, The Foundation na Asasi Wafadhiliwa watajaza hojaji ya kujitathmini zinazohusiana na Kanuni hizi na kuziwasilisha kwa the Foundation, Januari ya kila mwaka. Taarifa fupi ya majumuisho ya tathmini yatajadiliwa kwenye Tamasha la Kila Mwaka la AZAKi na pia kuchapishwa katika Jarida cha "the Foundarion News" na pia katika tovuti.
- The Foundation itasaidia Wafadhiliwa katika jitihada za kujengea uwezo juu ya kuimarisha utawala bora ndani ya AZAKi kupitia njia mbalimbali.
- Maofisa wa the Foundation, Washauri na Wabia wa maendeleo wanaweza kufuatilia uzingatiwaji wa Maadili haya wanapozitembelea Asasi Wafadhiliwa. Vivyo hivyo, Wafadhili wanaweza kuzitembelea ofisi za the Foundation ili kufuatilia uzingatiwaji wa Maadili haya ya Utawala Bora na Uwajibikaji.

4. Mapitio na Marekebisho (Revision)

- Marekebisho ya Kanuni hizi za Maadili yatahitaji mapendekezo ya theluthi mbili ya mashirika husika kama itakavyojidhihirisha katika fomu za kila mwaka za kujitathmini.